



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb.Na. HM/SI/T.41.91/29

26 Julai, 2022

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi 01 ya **Dereva Daraja la II**. Tangazo hili ni kutokana na Kibali cha Ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mchanganuo wa nafasi hiyo ni kama inavyoonekana hapa chini:-

### **1.0. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 01) TGS B**

#### **1.1. SIFA ZA MWOMBAJI.**

- Awe na Cheti cha ufaulu wa kidato cha Nne (IV) au VI.
- Awe na leseni ya daraja C au E ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au NIT au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

#### **1.2. KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA LA II**

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari na
- vi. Kufanya usafi wa gari.

#### **1.3. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 na usiopungua umri wa miaka 18.
- ii. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na Nakala ya kitambulisho cha Taifa (**NIDA**).

- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha Nne na kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- v. Picha ndogo moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vi. Testimonials "provisional Results" "Statement of results" Hati ya matokeo za kidato cha Nne na Sita, yaani **FORM IV NA FORM VI RESULTS SLIPS HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia waliopo katika Utumishi wa Umma **wasiombe kazi na wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyo katika waraka CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**
- viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza na yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida **kabla au ifikapo tarehe 09/08/2023 kwa njia ya Posta kwa anwani ifuatayo:-**

Imetolewa na :

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA  
S.L.P. 236,  
SINGIDA.**

Upendo Munyu Naftari  
**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA  
SINGIDA**

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
SINGIDA**

**Nakala:** Ubao wa Matangazo,  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P. 5,  
**SINGIDA**

“ Ubao wa Matangazo,  
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,  
S.L.P. 1  
**SINGIDA**